

Familia Pendwa za Shule za Umma za Kaunti ya Fayette:

Asante kwa yote munayofanya kwa kusaidia wanafunzi wenu na shule wakati hatuwezi kurudi salama kwa ujifunzaji wa uso-kwa-uso. Walimu wetu wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanapata uzoefu mzuri na wanajitaidi kwamba Mafundisho Isiyo ya Kawaida (NTI) 2DL iwe uboreshaji zaidi kuliko ile tuliyoifanya wakati wa msimu uliopita.

Shule zetu zitauliza maoni yenu kuhusu vile NTI: 2DL inaenda kwa familia yako. Ninakuhimiza ushiriki katika tafiti (surveys) hizi ili tuweze kurekebisha matoleo/mafundisho yetu kama ipasavyo.

Tunafanya kazi katika ushirika wa karibu pamoja na Idara ya Afya ya Kaunti ya Lexington-Fayette ili kujuwa kiwango cha sasa cha COVID-19 katika jamii yetu. Tuko katika mawasiliano ya kila siku na maafisa wa afya ili kujuwa viwango vya sasa vya matukio ya janga hili katika jamii yetu. Na tuna fuatilia pia kesi za wagonjwa miongoni mwa wanafunzi na wafanyikazi.

FCPS imegundua aina tatu za mafundisho inazoweza kutekelezwa kulingana na kiwango cha uenezi wa janga la COVID-19 na viwango cha maambukizo katika Kaunti ya Fayette:

- **Mfano 1: Shule ya Jadi au la Kawaida** – Mafundisho ya kibinafsi uso-kwa-uso pamoja na mazoea ya kuzuia, michakato na hatua.
- **Mfano 2: Mafundisho ya Mchangano** – Kuchanganya ratiba ya mafundisho ya uso-kwa-uso kibinafsi na mafundisho ya umbali.
- **Mfano 3: Mafundisho Yasiyo ya Kawaida (NTI)** - Majifunzo ya umbali katika shule au katika wilaya, kama inahitajika. Mpango ni kufunga sehemu Fulani na kusafisha maeneo yaliyoathiriwa. Kufunga shule lote kwa muda mfupi ili kuruhusu usafishaji wa jengo lote, au kufunga kwa muda mrefu, angalau siku 14.

Kutokana na taarifa ya Idara la Afya ya Kentucky, kwa sasa, Kaunti ya Fayette inatambua kuongezeka kwa sana kwa COVID-19. Tunahitaji jamii yetu yote itusaidie kupunguza idadi hizi kwa kufuata hatua zote za kupunguza zote za wanaafya, kwa mfano: umbali mbali wa kijamii na kuvaa barakoa. Unaweza kutusaidia kwa kufanya mambo haya mwenyewe, bali pia kwa kuhamasisha majirani zako, familia na marafiki kufanya vivyo hivyo.

Kama tulivyo wajulisha katika Kutafakari tena, Kufikiria upya na Kufanya upya mpango wa kurudi shuleni, tumeweka vipindi vya kila wiki 4 hadi 6 katika mwaka wote wa shule kutafakari ni mfano gani wa mafundisho unaofaa. Mda wetu wa kwanzawla ukaguzi umepangwa mwishoni mwezi huu.

Shule zetu zinajiandaa kikamilifu kwa kurudi kwa aina fulani ya mafundisho ya kibinafsi. Chapa za kubandika zinawekwa kwenye sakafu katika majengo yetu ya shule ili kuonyesha usalama kiafya kama vile; umbali mbali wa kijamii. Tumehifadhi shule zetu na vifaa sahihi vya kusafisha na vifaa vya kinga za kibinafsi, na samani (kama vile kabati) zinahamishwa darasani ili kuongeza nafasi.

Nimefurahi pia kuwajulisha kwamba wakati wa mkutano wa usiku wa leo wa Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Fayette, wanamemba wa bodi ya shule walikubali kununua Teknolojia ya Kuchukulia joto na Teknolojia ya Kugundua Joto kwa shule zetu za kati na za sekondari na kwa shule kubwa za msingi ili kutambua homa wakati halisi na kuchunguza joto. Hizi teknolojia ni sawa zile zilizo katika jengo ya Toyota pale Georgetown.

Ikiwa ungependa kusoma itifaki za kiafya na usalama tutakazozitekeleza tunaporudi shuleni, nimeziambatanisha na barua pepe hii. Napenda pia kuwahimiza mujizoeshe na ripoti yetu ya Kutafakari tena, Kufikiria upya na Kufanya upya, ambayo inapatikana katika lugha nyingi.

Kama baba na mwalimu, singependa chochote zaidi ya kurudi shuleni. Walakini, sio mahamuzi yangu. Kama vile Daktari Fauci alivyoeleza kwa busara miezi iliyopita, hatufanyi ratiba, "ni virusi vinavyofanya ratiba ya mda." Ninaomba msaada wako endelevu na ushirikiano wakati tunapitia pamoja nyakati hizi zenye changamoto.

Mshiriki weno,

Manny Caulk

Msimamizi wa Shule za Umma za Kaunti ya Fayette